TANGAZO LA SERIKALI Na. 935 La Tarehe 23/10/2020

SHERIA YA UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 292)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 116)*

KANUNI ZA MASHAURI YA UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA, 2020

## MPANGILIO WA KANUNI

*Kanuni* *Maelezo*

SEHEMU YA KWANZA
VIPENGELE VYA UTANGULIZI

1. Jina la Kanuni.
2. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
UWASILISHAJI WA SHAURI LA UCHAGUZI NA DHAMANA YA GHARAMA

3. Anayeweza kufungua shauri la uchaguzi.
4. Kupinga uchaguzi.
5. Muundo na maudhui ya hati ya shauri.
6. Wahusika katika shauri.
7. Kuongeza au kubadilisha wahusika katika shauri.
8. Kuwasilisha hati ya shauri.
9. Kuwasilisha na kupeleka nyaraka kwa njia ya kielektroniki.
10. Kukataliwa au kurekebishwa kwa hati ya shauri wakati wa uwasilishaji.
11. Kupeleka hati ya shauri na kuwasilisha majibu.
12. Dhamana ya gharama za shauri.

SEHEMU YA TATU
ORODHA YA KURA ZINAZOPINGWA NA MALALAMIKO DHIDI YA MATOKEO
YA UCHAGUZI KATIKA KITUO CHA UCHAGUZI

13. Orodha ya kura zinazopingwa.
14. Malalamiko dhidi ya matokeo ya uchaguzi katika kituo cha uchaguzi.
15. Kupanga tarehe ya kusikiliza shauri.

SEHEMU YA NNE
UTARATIBU WA KUSIKILIZA MASHAURI YA UCHAGUZI

16. Mahali na muda wa usikilizwaji wa shauri.
17. Kuunganisha mashauri.
18. Shauri kusikilizwa na zaidi ya hakimu mmoja.
19. Utoaji wa nyaraka.
20. Usikilizwaji wa awali.
21. Uainishaji wa hoja bishaniwa.
22. Matumizi ya Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai.
23. Usikilizwaji wa shauri.
24. Utaratibu wa kusikiliza shauri.
25. Shahidi wa mahakama.
26. Sababu zinazoweza kupokelewa wakati wa usikilizwaji.
27. Kuahirishwa kwa usikilizwaji washauri.
28. Katazo la kuahirisha shauri.
29. Hakimu kushindwa kuendelea na shauri.
30. Mleta shauri kushindwa kuhudhuria.
31. Mjibu shauri kushindwa kuhudhuria.
32. Kuhudhuria kupitia wakili.
33. Kuondoa shauri.
34. Ukomo kwa shauri.
35. Shauri kutotupiliwa mbali kwa sababu ya kasoro ya kiutaratibu.
36. Ada.
37. Kufutwa kwa Kanuni.

MAJEDWALI

TANGAZO LA SERIKALI Na. 783 Limetangazwa Tarehe 18 Septemba, 2020

SHERIA YA UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 292)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 116)*

KANUNI ZA MASHAURI YA UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA, 2020

## SEHEMU YA KWANZA
## VIPENGELE VYA UTANGULIZI

Jina la Kanuni

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Mashauri ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, 2020.

Tafsiri

2. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

Sura ya 292

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa;

Sura ya 11

"mahakama" maana yake ni mahakama ya Hakimu Mkazi kama ilivyotafsiriwa na Sheria ya Mahakama za Mahakimu na inajumuisha Mahakama ya Wilaya iliyoteuliwa kama Mahakama ya Hakimu Mkazi kwa madhumuni ya kusikiliza mashauri ya uchaguzi; na

"afisa uchaguzi" maana yake ni Msimamizi wa Uchaguzi, msimamizi wa kituo au afisa mwingine yeyote ambaye amepewa jukumu lolote rasmi na Sheria.

## SEHEMU YA PILI
## UWASILISHAJI WA SHAURI LA UCHAGUZI NA DHAMANA YA GHARAMA

Anayeweza kufungua shauri la uchaguzi

3. Mtu yeyote aliyeelezewa chini ya kifungu cha 110(1) cha Sheria anaweza kufungua shauri la uchaguzi.

Kupinga uchaguzi

4. Uchaguzi wa diwani utapingwa kwa njia ya shauri la uchaguzi.

Muundo na maudhui ya hati ya shauri

5.-(1) Kila hati ya shauri itakuwa na jina linaloshabihiana na Fomu A iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi na itaeleza:

(a) jina, maelezo na mahali anapoishi mleta shauri pamoja na anwani ya barua pepe, namba ya faksi, namba ya simu na msimbo wa posta iwapo zinapatikana;

(b) jina, maelezo na mahali anapoishi mjibu shauri pamoja na anwani ya barua pepe, nambaya faksi, namba ya simu na msimbo wa posta iwapo zinapatikana, kwa kadri inavyoweza kufahamika;

(c) sababu ambazo mleta shauri anazitegemea kwa ajili ya nafuu zinazoombwa; na

(d) nafuu inayoombwa au zinazoombwa na mleta shauri.

(2) Kila hati ya shauri itagawanywa katika aya zenye namba zinazofuatana, ambapo kila aya, kwa kadri inavyowezekana, itajikita katika maudhui tofauti.

Wahusika katika shauri

6.-(1) Katika kila shauri, Mwanasheria Mkuu wa Serikali atakuwa mmoja wa wajibu shauri isipokuwa kwa shauri lililowasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali mwenyewe.

(2) Endapo shauri lina madai yanayohusu mwenendo mbaya au ukiukwaji wa masharti ya Sheria yoyote au sheria yoyote uliofanywa na mgombea aliyeshinda au na mtu yeyote anayemuwakilisha au kwa niaba ya mgombea aliyeshinda, mgombea aliyeshinda ataunganishwa kama mhusika katika shauri pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

(3) Endapo shauri lina madai ya mwenendo mbaya au ukiukwaji wa masharti yoyote ya Sheria au sheria yoyote uliofanywa na afisa uchaguzi, afisa huyo wa uchaguzi ataunganishwa kama mhusika katika shauri pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

(4) Katika shauri lililowasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaweza kuwaunganisha kama wajibu shauri watu wote ambao wanaweza kuathiriwa ikiwa nafuu inayoombwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali itatolewa.

Kuongeza au kubadilisha wahusika katika shauri

7.-(1) Endapo mtu pekee aliyewekwa kuwa mhusika katika shauri ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kwa maoni ya mahakama ni vyema au muhimu kwa madhumuni ya kuamua masuala husika kwamba mgombea aliyeshindwa au mtu mwingine yeyote aunganishwe kuwa mhusika katika shauri, mahakama inaweza kutoa amri kuelekeza kwamba mgombea aliyeshindwa au mtu huyo mwingine aunganishwe kuwa mhusika katika shauri, na amri hiyo itakapotolewa shauri litaahirishwa hadi wakati ambapo mtu ambaye anapaswa kuunganishwa kuwa mhusika katika shauri amepewa nakala ya hati ya shauri.

(2) Endapo katika shauri lolote Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameunganishwa kama mhusika katika shauri na mgombea aliyeshindwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali akaishauri mahakama kwa maandishi kwamba hana maslahi na shauri hilo, mahakama inaweza kuelekeza kwamba Mwanasheria Mkuu wa Serikali atakoma kuwa mhusika katika shauri ikiwa imeridhika kuwa hakuna madai ya mwenendo mbaya kwa upande wa afisa yeyote wa uchaguzi, na shauri litaendelea kati ya mleta shauri na mjibu shauri au wajibu shauri waliobaki, kama inavyoweza kuwa.

Kuwasilisha hati ya shauri

8.-(1) Hati ya shauri itawasilishwa ndani ya mwezi mmoja tangu tarehe ya kutangazwa kwa matokeo kwa kuiwasilisha mahakamani na kwa kulipa ada iliyoainishwa.

(2) Shauri linaweza kuwasilishwa chini ya kanuni hii na mleta shauri mwenyewe au wakili wake.

(3) Mleta shauri atawasilisha kwa mahakama nakala tatu za nyaraka za hati ya na nakala za nyongeza kulingana na idadi ya wajibu maombi wanaohusika.

Kuwasilisha na kupeleka nyaraka kwa njia ya kielektroniki Tangazo la Serikali Na. 148 la 2018

9. Endapo Kanuni hizi zinahitaji nyaraka kuwasilishwa katika mahakama au kupelekwa kwa mhusika, uwasilishaji au upelekaji huo, kama inavyoweza kuwa, unaweza kufanyika kwa njia ya kielektroniki na Kanuni za Matumizi ya Sheria (Uwasilishaji Nyaraka Mahakamani kwa Njia ya Kielektroniki), zitatumika kwa kuzingatia maboresho muhimu kwa kadri itakavyohitajika.

Kukataliwa au kurekebishwa kwa hati ya shauri wakati wa uwasilishaji

10.-(1) Endapo hati ya shauri haijaandaliwa kwa namna ilivyoainishwa awali, inaweza kukataliwa na kurudishwa kwa mleta shauri kwa madhumuni ya kurekebishwa ndani ya muda utakaopangwa na mahakama.

(2) Endapo mahakama itakataa hati ya shauri lolote, ataandika katika hati ya shauri hilo sababu za kukataliwa na tarehe ya kuwasilishwa na kukataliwa.

(3) Mtu yeyote asiyeridhika na uamuzi wa mahakama wa kukataa hati ya shauri chini ya kanuni hii anaweza kupeleka maombi ya masahihisho Mahakama Kuu kwa uamuzi wa upande mmoja utakaotolewa ndani ya siku nne za kuwasilishwa kwa maombi ya masahihisho.

(4) Maombi chini ya kanuni ndogo ya (3) yanaweza kuwasilishwa kwa njia isiyo rasmi:

(a) kwa mdomo wakati uamuzi unatolewa; au
(b) kwa maandishi ndani ya siku saba za uamuzi.

(5) Endapo uamuzi wa mahakama utabadilishwa na Mahakama Kuu, mleta shauri anaweza kuwasilisha tena hati ya shauri lake na muda uliotumika tangu wakati alipowasilisha shauri lililokataliwa mpaka uamuzi wa Mahakama Kuu katika maombi ya masahihisho ulipotolewa hautajumuishwa katika kuhesabu muda wa kufungua shauri chini ya kifungu cha 114(1) cha Sheria.

Kupeleka hati ya shauri na

11.-(1) Endapo hati ya shauri imewasilishwa na haijakataliwa au kurudishwa kwa mleta shauri,

kuwasilisha majibu

mahakama ndani ya siku tano:

(a) itatuma kwa afisa uchaguzi nakala ya hati ya shauri pamoja na notisi iliyoainishwa katika Fomu B iliyopo katika Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi;

(b) itaagiza kila mjibu shauri kupelekewa nakala ya hati ya shauri pamoja na notisi iliyoainishwa katika Fomu C iliyopo katika Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi;

(c) itabandika katika ubao wa matangazo wa mahakama nakala ya hati ya shauri iliyothibitishwa.

(2) Upelekaji wa nyaraka zilizotajwa katika kanuni ndogo ya (1)(b) utakuwa kwa njia ya makabidhiano binafsi.

(3) Endapo mahakama imeridhika kwamba-

(a) mjibu shauri hawezi kupatikana;

(b) mjibu shauri amekataa kupokea nyaraka;

(c) makabidhiano binafsi hayawezi kufanyika bila kucheleweshwa au bila gharama kubwa; au

(d) ni vyema kufanya hivyo,

inaweza kuelekeza upelekaji wa nyaraka ufanyike kwa njia mbadala kwa namna ambayo mahakama inaweza kuelekeza.

(4) Isipokuwa kama mjibu shauri hana nia ya kupinga shauri hilo, mara atakapopelekewa nakala ya hati ya shauri, atawasilisha mahakamani majibu yake ndani ya siku kumi na nne tangu tarehe ya kupelekewa hati ya shauri.

Dhamana ya gharama za shauri

12.-(1) Mleta shauri, ndani ya siku kumi na nne baada ya kufungua shauri, atapeleka maombi kwa ajili uamuzi wa kiwango kinachopaswa kulipwa kama dhamana ya gharama za shauri.

(2) Utaratibu wa kuweka dhamana ya gharama za shauri utakuwa kama ulivyoainishwa chini ya kifungu cha 110 cha Sheria.

(3) Endapo mleta shauri ana uwezo wa kifedha na yuko tayari kuweka shilingi laki tano ambacho ni

kiwango cha juu cha dhamana ya gharama za shauri zilizoainishwa chini ya kifungu cha 110(2) cha Sheria, hatahitajika kupeleka maombi kwa ajili ya uamuzi wa kiwango kinachopaswa kulipwa kama dhamana ya gharama za shauri chini ya kifungu cha 110(3) cha Sheria ila lakini ataweka kiwango hicho ndani ya siku kumi na nne tangu kufungua shauri.

Sura ya 21

(4) Hakuna dhamana ya gharama za shauri itakayolipwa na mleta shauri ambaye amepewa msaada wa kisheria chini ya Sheria ya Msaada wa Kisheria.

## SEHEMU YA TATU
## ORODHA YA KURA ZINAZOPINGWA NA MALALAMIKO DHIDI YA MATOKEO YA UCHAGUZI KATIKA KITUO CHA UCHAGUZI

Orodha ya kura zinazopingwa

13.-(1) Endapo uchunguzi unaombwa na mleta shauri au mjibu shauri chini ya masharti ya aya (d) ya kifungu cha 115 cha Sheria, mhusika anayeomba uchunguzi huo atawasilisha mahakamani orodha ya kura anazokusudia kuzipinga na pingamizi kwa kila kura, ndani ya siku zisizopungua sita kabla ya siku iliyopangwa kwa ajili ya usikilizwaji wa shauri, na hakuna ushahidi utakaotolewa wakati wa usikilizwaji wa shauri dhidi ya uhalali wa kura yoyote au kuunga mkono pingamizi lolote ambalo halijaainishwa kwenye orodha hiyo, isipokuwa kwa ruhusa ya mahakama na kwa masharti ambayo mahakama inaweza kuamuru.

(2) Mhusika anayewasilisha orodha kwa mujibu wa masharti ya kanuni ndogo ya (1) atawasilisha mahakamani kwa wakati mmoja nakala mbili za orodha hiyo na nakala za nyongeza kulingana na idadi ya wahusika katika shauri.

(3) Mahakama itaagiza nakala ya orodha hiyo kutumwa kwa Msimamizi wa Uchaguzi na kwa kila mhusika mwingine katika shauri.

Malalamiko dhidi ya matokeo ya uchaguzi katika kituo cha

14.-(1) Endapo mleta shauri anadai kwamba, mgombea mwingine yeyote tofauti na mjibu shauri alichaguliwa kihalali, atawasilisha mahakamani orodha ya matokeo ya uchaguzi ya kituo cha kupigia kura

uchaguzi

anayokusudia kuyatumia ndani ya siku zisizopungua sita kabla ya siku iliyopangwa kwa ajili ya usikilizwaji wa shauri.

(2) Endapo mleta shauri amewasilisha mahakamani orodha kwa mujibu wa masharti ya kanuni ndogo ya (1), atawasilisha kwa mahakama nakala mbili za orodha hiyo na nakala za nyongeza kulingana na idadi ya wahusika katika shauri.

(3) Mahakama itaagiza nakala ya orodha hiyo kutumwa kwa Msimamizi wa Uchaguzi na kwa kila mhusika mwingine katika shauri

(4) Hakuna mleta shauri atakayesikilizwa juu ya sababu yoyote ya malalamiko ambayo haijaainishwa katika orodha inayotakiwa kuwasilishwa chini ya kanuni hii, isipokuwa kwa ruhusa ya mahakama na kwa masharti ambayo mahakama inaweza kuamuru

Kupanga tarehe ya kusikiliza shauri

15.-(1) Kwa kuzingatia Kanuni hizi, baada ya kukamilika kwa uwasilishwaji wa nyaraka za shauri, mahakama itawapangia mapema iwezekanavyo wahusika wote au mawakili wao kufika mbele ya mahakama kwa madhumuni ya kupanga tarehe ya kusikilizwa kwa shauri.

(2) Endapo mhusika yeyote katika shauri atashindwa kufika mbele ya mahakama baada ya kutakiwa kufanya hivyo, mahakama itaendelea kupanga tarehe ya usikilizwaji bila uwepo wa mhusika huyo na itamtaarifu mhusika huyo kwa maandishi tarehe ya usikilizwaji iliyopangwa.

(3) Bila kujali masharti mengine yoyote ya Kanuni hizi, endapo suala linapaswa kusikilizwa au endapo wahusika wanapaswa kufika mbele ya mahakama, usikilizwaji huo au kufika huko, kama inavyoweza kuwa, kunaweza kuwa kwa njia ya:

(a) mfumo wa mkutano kwa video unaomilikiwa au ulioidhinishwa na Mahakama ya Tanzania; au

(b) mkutano kwa simu.

Sura ya 6

(4) Usikilizwaji wa shauri kwa njia ya mkutano kwa video au mkutano kwa simu utakuwa kwa mujibu

wa Sheria ya Ushahidi.

## SEHEMU YA NNE
## UTARATIBU WA KUSIKILIZA MASHAURI YA UCHAGUZI

Mahali na muda wa usikilizwaji wa shauri
Sura ya 11

16.-(1) Kwa dhumuni la kushughulikia mashauri ya uchaguzi, Jaji Mkuu anaweza, kwa mujibu wa kifungu cha 5(1) cha Sheria ya Mahakama za Mahakimu, kufanya uteuzi mahsusi wa mahakama yoyote ya wilaya kuwa Mahakama ya Hakimu Mkazi.

(2) Usikilizwaji wa shauri utafanyika muda na mahali kadri mahakama inavyoweza kuamua.

(3) Mahakama itatoa notisi ya siku, muda na mahali ambapo shauri litasikilizwa kwa kila mhusika wa shauri na kubandika notisi hiyo kwenye ubao wa matangazo wa mahakama au kutangaza katika magazeti kama mahakama inavyoweza kuelekeza.

(4) Kila shauri litasikilizwa katika mahakama ya wazi.

Kuunganisha mashauri

17. Endapo mashauri mawili au zaidi yamewasilishwa kuhusiana na uchaguzi mmoja, mahakama inaweza kuelekeza kwamba baadhi au mashauri hayo yote yaunganishwe na kusikilizwa kama shauri moja.

Shauri kusikilizwa na zaidi ya hakimu mmoja

18.-(1) Endapo, kwa maoni ya Jaji Mkuu, shauri linaweza kuibua hoja ngumu za kisheria au zisizo za kisheria au zote kwa pamoja, anaweza kuelekeza kuwa shauri hilo lisikilizwe na zaidi ya hakimu mmoja.

(2) Pale shauri linaposikilizwa na zaidi ya hakimu mmoja, litaamuliwa kulingana na maamuzi ya mahakimu walio wengi.

Utoaji wa nyaraka

19.-(1) Wahusika katika shauri au mawakili wao, wakati shauri linasikilizwa kwa mara ya kwanza, watatoa ushahidi wote wa nyaraka wa kila aina ulio katika milki au mamlaka yao, ambao wanakusudia kuutegemea na ambao bado haujawasilishwa mahakamani, na nyaraka zote ambazo mahakama imeamuru zitolewe.

(2) Mahakama itapokea nyaraka zilizotolewa ikiwa tu zimeambatana na orodha sahihi iliyoandaliwa katika namna ambayo mahakama inaweza kuelekeza.

Sura ya 33

(3) Utaratibu wa utoaji wa nyaraka utasimamiwa, kwa karibu kadri iwezekanavyo, kwa kuzingatia wa Amri ya XIII ya Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai.

Usikilizwaji wa awali

20.-(1) Mara baada ya kukamilika kwa uwasilishwaji wa nyaraka za shauri, mahakama itafanya usikilizwaji wa awali mbele ya wahusika au mawakili wao ili kuainisha masuala yasiyobishaniwa kati ya wahusika wa shauri na yatakayowezesha usikilizwaji wa shauri kwa haki na haraka.

(2) Mahakama itajiridhisha kutoka kwa wahusika na kupitia nyaraka za shauri masuala ya kisheria au yasiyo ya kisheria yasiyobishaniwa.

(3) Mwishoni mwa usikilizwaji wa awali uliofanyika chini ya kanuni hii, mahakama itaandaa hati ya masuala yasiyobishaniwa na hati hiyo itasomwa na kuelezewa kwa wahusika wa shauri au mawakili wao.

(4) Hati iliyoandaliwa chini ya kanuni ndogo ya (3) itasainiwa na wahusika wa shauri au mawakili wao pamoja na hakimu.

(5) Suala lolote au nyaraka yoyote iliyokubaliwa na kuainishwa katika hati iliyoandaliwa chini ya kanuni hii vitachukuliwa kuwa vimethibitishwa; isipokuwa kama, wakati wa usikilizwaji wa shauri, mahakama ina maoni kwamba maslahi ya haki yanahitaji hivyo, inaweza kuelekeza kwamba suala lililokubaliwa au nyaraka iliyopokelewa katika hati iliyoandaliwa chini ya kanuni hii vithibitishwe rasmi.

Uainishaji wa hoja bishaniwa

21-(1) Baada ya usikilizwaji wa awali kukamilika, mahakama itaainisha masuala ambayo wahusika wa shauri wanabishania na kuandika hoja bishaniwa ambazo uamuzi sahihi wa shauri unaonekana kuzitegemea.

Sura ya 33

(2) Uainishaji wa hoja bishaniwa utasimamiwa, kwa karibu kadri iwezekanavyo, kwa kuzingatia Amri ya XIV ya Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai.

Matumizi ya Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai Sura ya 33

22.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria na Kanuni hizi, usikilizwaji, utaratibu na mwenendo wa shauri utasimamiwa, kwa karibu iwezekanavyo, na kanuni zinazosimamia utaratibu na mwenendo wa mashauri ya madai.

(2) Bila kuathiri ujumla wa masharti ya kanuni ndogo ya (1), masharti ya Jedwali la Kwanza la Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai, yanayohusu ugunduzi na ukaguzi wa nyaraka, kiri, utoaji, kushikiliwa na kurudishwa kwa nyaraka, uhamishaji wa mashauri, utatuzi wa hoja na uamuzi wa mashauri, wito wa mashahidi, kupokelewa kwa hati za kiapo, utoaji wa gharama za shauri, hukumu na utekelezaji wa amri, yatatumika kwa kuzingatia maboresho muhimu kwa kadri yatakavyohitajika katika mwenendo wa usikilizwaji wa shauri na katika utekelezaji wa amri ya kulipa gharama za shauri iliyotolewa na mahakama.

Usikilizwaji wa shauri

23.-(1) Usikilizwaji wa mashauri ya uchaguzi mbele ya mahakama utakuwa kwa njia ya maelezo ya maandishi ya mashahidi badala ya ushahidi wa msingi wa kuhojiwa.

(2) Mashahidi wataitwa na kuapishwa kwa namna sawa kadri hali inavyoruhusu, kama ilivyo katika usikilizwaji wa mashauri ya madai na mahakama katika utekelezaji wa mamlaka yake ya awali, na bila kuathiri masharti ya sheria nyingine yoyote, watawajibika kwa adhabu zile zile kwa kutoa ushahidi wa uwongo au kwa kutohudhuria mahakamani.

(3) Baada ya usikilizwaji wa awali, mleta shauri atawasilisha katika ofisi ya mahakama maelezo ya maandishi ya kila shahidi ambaye mleta anakusudia kumuita wakati wa usikilizwaji yakielezea msingi wa ushahidi wake ndani ya saa zisizopungua arobaini na nane kabla ya muda uliopangwa na mahakama wa kusikiliza shauri la uchaguzi.

(4) Mjibu shauri, ndani ya saa arobaini na nane za kufungwa kwa shauri la upande wa mleta shauri, atawasilisha katika ofisi ya mahakama maelezo ya maandishi ya kila shahidi anayekusudia kumuita wakati

wa utetezi, yakielezea msingi wa ushahidi wake.

(5) Maelezo ya maandishi ya shahidi chini ya kanuni hii:

(a) yatatolewa kwa kiapo au uthibitisho;
(b) yatajumuisha jina, umri, anwani na kazi ya shahidi;
(c) kwa kadri inavyowezekana, yatakuwa katika maneno ya shahidi aliyekusudiwa;
(d) yatatambua kikamilifu nyaraka yoyote inayorejewa katika maelezo bila kurudia yaliyomo isipokuwa kama ni muhimu ili kuitambua nyaraka husika;
(e) hayatajumuisha masuala ya kutaarifiwa au imani ambayo hayawezi kupokelewa na endapo yanaweza kupokelewa, yataelezea chanzo cha taarifa au imani;
(f) hayatakuwa na nukuu ndefu kutoka katika nyaraka au kujikita katika hoja za kisheria au nyinginezo;
(g) yatajumuisha tamko la shahidi aliyekusudiwa kwamba anaamini maelezo ya hali halisi katika maelezo hayo ni ya kweli;
(h) yatawekwa tarehe na kusainiwa au kuthibitishwa vinginevyo na shahidi aliyekusudiwa;
(i) yatakuwa katika aya zilizo na namba; na
(j) yatakuwa katika lugha ya mahakama.

(6) Ikiwa shahidi haelewi lugha ya mahakama vizuri, lakini anaweza kujieleza na kueleweka na anaweza kuelewa lugha ya mahakama iliyo katika maandishi, maelezo yake yanaweza yasiwe katika maneno yake mwenyewe:

Isipokuwa kwamba, masuala haya yawe yameainishwa katika maelezo yenyewe na kuandikwa ili kuelezea kwa usahihi iwezekanavyo msingi wa ushahidi wake.

(7) Maelezo ya maandishi ya shahidi yatashabihiana na Fomu D iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi.

(8) Maelezo ya maandishi ya kila shahidi

yatawekwa katika bahasha iliyofungwa pamoja na nakala za kutosha zilizothibitishwa kama nakala halisi kwa ajili ya kila hakimu, waleta shauri wengine wote katika shauri hilo na wajibu shauri, na yatafunguliwa na mahakama wakati shahidi aliyetoa maelezo ameitwa kutoa ushahidi.

Utaratibu wa kusikiliza shauri

24.-(1) Mhusika wa shauri ambaye kwa niaba yake maelezo ya maandishi ya shahidi yamewasilishwa atahakikisha kuwa shahidi wake anahudhuria wakati wa usikilizwaji kwa madhumuni ya kutoa rasmi maelezo yake na kuwasilisha vielelezo, kama vipo.

(2) Pale ambapo shahidi amehudhuria kwa ajili ya utoaji rasmi wa maelezo yake na uwasilishaji wa vielelezo, ataapishwa kwa namna iliyoainishwa na sheria inayotumika katika kuapisha mashahidi.

(3) Mara baada ya maelezo ya maandishi ya shahidi kutolewa rasmi mahakamani, yatakuwa sehemu ya kumbukumbu ya usikilizwaji wa shauri na yatasomwa kwa sauti kubwa na au kwa niaba ya shahidi.

(4) Shahidi ambaye maelezo yake yametolewa rasmi anaweza kuhojiwa na upande wa pili wa shauri na kuhojiwa tena na upande ulimuita kutoa ushahidi.

(5) Shahidi ambaye maelezo yake hayajatolewa chini ya kanuni ya 23(3), (4) au yametolewa kinyume na kanuni ya 23(8) hataruhusiwa kutoa ushahidi bila idhini ya mahakama, na mahakama haitatoa idhini hiyo isipokuwa kama ameonesha sababu za msingi za kushindwa huko.

Shahidi wa mahakama

25.-(1) Wakati wa usikilizwaji wa shauri la uchaguzi chini ya Sheria, mahakama inaweza:

(a) kutoa amri, kumtaka mtu yeyote ambaye inaona kuwa amehusika katika uchaguzi unahusiana na shauri kuhudhuria kama shahidi; na
(b) kumhoji shahidi yeyote aliyetakiwa kuhudhuria chini ya kanuni ndogo ya (1) na baada ya kuhojiwa kwa shahidi huyo na mahakama, shahidi huyo anaweza kuhojiwa

na au kwa niaba ya mleta shauri, mjibu shauri na Mwanasheria Mkuu wa Serikali au mwakilishi wake, ikiwa yupo, au yeyote kati yao.

Sura ya 16

(2) Mtu anayekataa kutii amri ya mahakama chini ya kanuni ndogo ya (1)(a) atakuwa ametenda kosa la kuidharau mahakama chini ya Sheria ya Kanuni ya Adhabu.

(3) Masharti ya kanuni ya 23 na 24 ya Kanuni hizi hayatatumika kwa shahidi aliyeitwa na mahakama chini ya kanuni hii.

Sababu zinazoweza kupokelewa wakati wa usikilizwaji

26. Isipokuwa kwa ruhusa ya mahakama, mleta shauri hataleta hoja au kusikilizwa kuhusiana na sababu yoyote ambayo haikuainishwa katika hati ya shauri.

Kuahirishwa kwa usikilizwaji wa shauri

27.-(1) Mahakama kwa amri iliyotolewa baada ya maombi ya mhusika katika shauri na kuungwa mkono na hati ya kiapo, na baada ya notisi kwa wahusika wengine katika shauri au kwa maamuzi yake yenyewe kwa notisi katika namna inayoweza kuamuru, inaweza kuahirisha kuanza kwa usikilizwaji wa shauri mpaka siku ambayo inaweza kuelekeza.

(2) Nakala ya notisi na ya amri iliyotolewa chini ya masharti ya kanuni ndogo ya (1) zitatumwa na mahakama kwa kila mhusika katika shauri na nakala nyingine itabandikwa kwenye ubao wa matangazo wa mahakama.

(3) Pale ambapo kwa sababu ya kutokuwepo kwa hakimu, usikilizwaji wa shauri hauwezi kuanza au endapo umeanza, hauwezi kuendelea kwa siku iliyopangwa kwa ajili ya usikilizwaji huo au kuendelea na usikilizwaji huo, usikilizwaji wa shauri hilo utaahirishwa hadi siku inayofuata, au tarehe yoyote inayofaa kwa mahakama hadi hapo hakimu atakapopatikana kusikiliza shauri hilo.

(4) Endapo kuanza kwa usikilizwaji wa shauri kumeahirishwa chini ya masharti ya kanuni ndogo ya (3) na hakuna uwezekano kuwa hakimu aliyepangiwa shauri hilo atapatikana ndani ya siku thelathini zijazo,

hakimu mwingine atapangiwa kuendelea na usikilizwaji huo.

Katazo la kuahirisha shauri

28. Usikilizwaji wa shauri unapoanza, utaendelea siku hadi siku mpaka mashahidi wote waliohudhuria watakapohojiwa, isipokuwa kama mahakama itaona kuwa kuahirishwa kwa usikilizwaji zaidi ya siku inayofuata ni muhimu kwa sababu zitakazoandikwa katika mwenendo wa shauri.

Hakimu kushindwa kuendelea na shauri

29.-(1) Endapo hakimu ambaye ameanza kusikiliza shauri atashindwa kumalizia uamuzi wa shauri kwa sababu ya ugonjwa, kifo au sababu nyingine ya msingi, hakimu mwingine anaweza kupangiwa shauri hilo ndani ya siku saba na hakimu huyo aliyepokea shauri anaweza kushughulikia ushahidi wowote au hati iliyopokelewa kama vilevile ushahidi huo au hati hiyo imepokelewa au kuandaliwa na yeye mwenyewe na anaweza kuendelea na shauri hilo kuanzia kwenye hatua ambayo mtangulizi wake aliishia.

(2) Hakimu aliyepokea shauri ataandika sababu za kupokea shauri hilo kabla ya kuendelea na usikilizwaji.

Mleta shauri kushindwa kuhudhuria

30.-(1) Endapo mleta shauri atashindwa kufika mbele ya mahakama wakati shauri limeitwa kwa ajili ya usikilizwaji, mahakama inaweza kutupilia mbali shauri hilo.

(2) Endapo shauri limetupiliwa mbali chini ya kanuni ndogo ya (1) mahakama inaweza, baada ya maombi kuletwa ndani ya siku kumi na nne tangu kutupiliwa mbali, kulirejesha shauri ikiwa mleta shauri atairidhisha mahakama kwamba kutofika kwake siku ya usikilizwaji kulitokana na sababu ya msingi.

Mjibu shauri kushindwa kuhudhuria

31.-(1) Endapo mjibu shauri atashindwa kufika mbele ya mahakama wakati shauri limeitwa kwa ajili ya usikilizwaji, mahakama inaweza kuendelea na kusikiliza shauri hilo bila uwepo wake.

(2) Mjibu shauri ambaye amri au uamuzi wa upande mmoja umetolewa dhidi yake atakuwa na haki

*Tangazo la Serikali Na. 935 (Linaendelea.)*

ya kufanya maombi ya kutengua amri au uamuzi wa upande mmoja ndani ya siku kumi na nne tangu amri hiyo au uamuzi huo kutolewa.

Kuhudhuria kupitia wakili

32. Kwa madhumuni ya Kanuni hizi, kuhudhuria kwa wakili kutachukuliwa kuwa ni kuhudhuria kwa mhusika wa shauri anayewakilishwa.

Kuondoa shauri

33-(1) Mleta shauri anaweza, kwa notisi ya maandishi kwenda kwa mahakama, kuondoa shauri wakati wowote baada ya shauri kufunguliwa na kabla ya uamuzi kutolewa, kwa kuzingatia masharti yanayohusiana na gharama za shauri ambazo mahakama inaweza kuona inafaa kuamuru.

(2) Endapo mleta shauri ataondoa shauri, hatakuwa na haki ya kufungua shauri jipya kuhusiana na uchaguzi huo huo:

Isipokuwa kwamba, mahakama inaweza kumruhusu mleta shauri kufungua shauri jipya kuhusiana na uchaguzi huo huo kwa kuzingatia sheria ya ukomo, endapo mahakama imejiridhisha kuwa shauri liliondolewa kwa sababu ambayo ingefanya shauri hilo kushindwa kwa hoja ya kasoro yoyote ya kiutaratibu.

(3) Endapo kuna waleta shauri wawili au zaidi, shauri hilo halitaondolewa isipokuwa kwa maombi ya maandishi ya waleta shauri wote.

Ukomo wa shauri

34.-(1) Shauri litakoma baada ya:

(a) kifo cha mleta shauri aliyekuwa mhusika pekee au mleta shauri pekee aliyekuwa amebaki hai; au

(b) kifo cha mgombea aliyeshinda.

(2) Endapo shauri litakoma kwa sababu ya kifo cha mleta shauri aliyekuwa mhusika pekee au mleta shauri pekee aliyekuwa amebaki hai mahakama inaweza, ikiwa itaona ni sawa na haki kufanya hivyo, kumpa mjibu shauri au, endapo kuna wajibu shauri wawili au zaidi, kila mjibu shauri, gharama za shauri ambazo mahakama inaweza kuona inafaa:

Isipokuwa kwamba, kiwango cha gharama za shauri atakazopewa mjibu shauri chini ya aya hii

hakitazidi kiwango cha gharama za shauri ambacho mleta shauri aliweka kama dhamana kwa ajili ya mjibu shauri huyo.

Shauri kutotupiliwa mbali kwa sababu ya kasoro ya kiutaratibu

35.-(1) Isipokuwa kama imeelezwa vinginevyo katika Kanuni hizi, hakuna shauri litakalotupiliwa mbali kwa sababu tu ya kutozingatia masharti yoyote ya Kanuni hizi au kasoro nyingine yoyote ya kiutaratibu isipokuwa kama mahakama ina maoni kwamba kutozingatia huko au kasoro hiyo imesababisha au inaweza kusababisha kupotea kwa haki.

(2) Endapo masharti yoyote ya Kanuni hizi hayajazingatiwa au kumekuwa na kasoro nyingine yoyote ya kiutaratibu, mahakama inaweza kumtaka mleta shauri kurekebisha kutozingatia huko au kasoro hiyo kwa namna ambayo mahakama inaweza kuamuru kwa kuzingatia masharti ya gharama za shauri au vinginevyo kama ambavyo mahakama inaweza kuamuru.

(3) Endapo amri imetolewa chini ya kanuni ndogo ya (2) ya kanuni hii, na mleta shauri akashindwa kuzingatia amri hiyo ndani ya muda unaoweza kuainishwa na mahakama, mahakama inaweza kufukuza shauri hilo.

Ada

36.-(1) Ada za mahakama zitalipwa kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Kanuni hizi.

Sura ya 21

(2) Hakuna ada itakayolipwa na mhusika wa shauri ambaye amepewa msaada wa kisheria chini ya Sheria ya Msaada wa Kisheria.

Kufutwa kwa Kanuni Tangazo la Serikali Na. 448 la mwaka 2010

37. Kanuni za Mamlaka za Mitaa (Mashauri ya Uchaguzi) za mwaka 2010 zinafutwa.

FOMU A

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 5, 11 na 23)*

KATIKA MAHAKAMA TEULE /* MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI YA

………..........................................................................................………………

MAHALI..................................................................................................................

SHAURI LA UCHAGUZI NA… ....... LA MWAKA 20……....

Katika Shauri la Uchaguzi chini ya Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Sura ya 292 na Kanuni za Mashauri ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa za mwaka 2020.

......................................................................................... Mleta shauri/ Waleta shauri

dhidi ya

..... ...................................................................................Mjibu shauri/ Wajibu shauri

HATI YA SHAURI LA UCHAGUZI
[Kanuni ya 5(1)]

Endapo Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni mhusika katika shauri, cheo chake pekee cha "Mwanasheria Mkuu wa Serikali" ndicho kitakachotajwa.

**Futa isiyohusika*

FOMU B

KATIKA MAHAKAMA TEULE /* MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI YA

………...……………………………………………………………………………….

MAHALI..........................................................................................................................

SHAURI LA UCHAGUZI NA… ....... LA MWAKA 20…….....

Katika Shauri la Uchaguzi chini ya Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Sura ya 292 na Kanuni za Mashauri ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa za mwaka 2020.

........................................................................................ Mleta shauri/ Waleta shauri
dhidi ya
..... ..................................................................................Mjibu shauri/ Wajibu shauri

NOTISI YA KUFUNGUA SHAURI LA UCHAGUZI
[Kanuni ya 11(1)(a)]

Kwa: Mkurugenzi wa Uchaguzi,
Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

DODOMA

Unataarifiwa kuwa shauri hili, ambalo nakala ya hati yake imeambatishwa pamoja na notisi hii, lilifunguliwa katika Mahakama ya …………................. ya …………………….. tarehe ................ 20 .........

Tarehe ....... ................ 20 .............

.................................................... Hakimu Mkazi.

**Futa isiyohusika*

FOMU C

KATIKA MAHAKAMA TEULE /* MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI YA

………...…………………………………………………………………………………

MAHALI...........................................................................................................

SHAURI LA UCHAGUZI NA… ....... LA MWAKA 20……......

Katika Shauri la Uchaguzi chini ya Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Sura ya 292 na Kanuni za Mashauri ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa za mwaka 2020.

........................................................................................ Mleta shauri/ Waleta shauri

dhidi ya

..... ..................................................................................Mjibu shauri/ Wajibu shauri

NOTISI YA KUWASILISHA MAJIBU YA SHAURI LA UCHAGUZI NA KUHUDHURIA

[Kanuni ya 11(1)(b)]

Kwa: ..........................................................................................................................

...........................................................................................................................................

.............................................................. (Jina na Anwani ya Mjibu shauri).

Unataarifiwa kuwa shauri hili, ambalo nakala ya hati yake imeambatishwa pamoja na notisi hii, lilifunguliwa katika Mahakama hii tarehe ................ 20 .........

Unatakiwa kuwasilisha majibu ya shauri hilo ndani ya siku kumi na nne tangu tarehe ya kupokea nakala ya hati ya shauri na kufika mbele yangu katika Mahakama ya………………………..………. tarehe ………………….. saa ………………….kamili mchana kwa madhumuni ya kupanga tarehe ya usikilizwaji wa shauri.

Tarehe ....... ................ ............................................

Hakimu Mkazi Mfawidhi

Nakala kwa: (Jina na Anwani ya Mleta shauri).

**Futa isiyohusika*

FOMU D

KATIKA MAHAKAMA TEULE /* MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI YA

………...…………………………………………………………………………………….

MAHALI..............................................................................

SHAURI LA UCHAGUZI NA. ........ LA MWAKA 20……......

Katika Shauri la Uchaguzi chini ya Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Sura ya 292 na Kanuni za Mashauri ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa za mwaka 2020.

....................................................................................... Mleta shauri/ Waleta shauri
dhidi ya
......................................................................................Mjibu shauri/ Wajibu shauri

MAELEZO YA MAANDISHI YA SHAHIDI
[Kanuni ya 23(7)]

Kwa ajili ya ……………..………. (Andika jina la mhusika ambaye maelezo yanatolewa kwa ajili yake)
Yametolewa na: Bw/Bibi/Bi
……………………………………………………………................
wa
S.L.P………………………………………………………………………………………
Maelezo ya shahidi wa Kwanza/ Pili/ Tatu/ Nne/ Tano/ Sita

………………………………………………………………………………………….
Nyaraka/vitu vinavyorejewa

………………………………………………………………………………………….

Tarehe ……………..………………………………

1. Kiini cha Maelezo ya Shahidi

1.1. Isipokuwa kama haiwezekani, maelezo ya shahidi yatakuwa katika maneno ya shahidi aliyekusudiwa, maelezo hayo yatatolewa katika nafsi ya kwanza na yataeleza:
   (a) Jina kamili la shahidi, makazi yake na ikiwa anatoa maelezo hayo kwa taaluma yake, au kwa wadhifa wake mwingine, anwani ya mahali pa kazi, nafasi anayoshika na jina la kampuni yake au mwajiri; na
   (b) Kwamba yeye ni mhusika katika shauri.

2. Maelezo ya shahidi yataonyesha:
   (a) Ni maelezo yanatokana na uelewa binafsi wa shahidi mwenyewe na ambayo ni masuala ya kutaarifiwa au imani; na
   (b) Chanzo cha taarifa au msingi wa imani katika aya husika.

3. Rejea ya nyaraka / vitu

3.1. Nyaraka/vitu vilivyotumika pamoja na maelezo ya shahidi vitathibitishwa na kutambuliwa na shahidi na kutenganishwa na maelezo ya shahidi.

3.2. Endapo shahidi anarejea nyaraka/kitu, ataeleza '"Ninarejea (maelezo ya nyaraka/kitu) iliyowekwa alama ...................... ......................... ".

3.3. Kwenye kona ya juu kulia katika ukurasa wa kwanza (na katika ukurasa wa nyuma) wa kila nyaraka /kitu kutaandikwa kwa ufasaha:
   (a) mhusika wa shauri ambaye maelezo hayo yanakusudiwa kutolewa kwa niaba yake;
   (b) herufi za mwanzo za jina na jina la ukoo la shahidi;
   (c) nambaya maelezo kuhusiana na shahidi husika; na
   (d) herufi na nambaza utambulisho za kila nyaraka/ kitu kilichorejewa.

3.4. Endapo shahidi atatoa maelezo zaidi ya mara moja ambayo yana nyaraka/vitu, katika shauri hilo hilo, nambakatika nyaraka/vitu zitafuatana mfululizo na hazitaanza upya kwa kila maelezo ya shahidi.

4. Muundo wa maelezo ya shahidi

4.1. Maelezo ya shahidi:
   (a) yatatolewa katika karatasi ya A4 yenye ubora madhubuti yenye mstari wa pambizo wa sentimita 3.5;
   (b) yatasomeka kikamilifu na kwa kawaida yatachapishwa katika upande mmoja tu wa karatasi;
   (c) pale itakapowezekana, yatafungwa kwa usalama kwa namna ambayo haitakwamisha kuweka kwenye jalada, au vinginevyo kila ukurasa utaandikwa namba ya shauri na kuwekwa herufi za mwanzo za majina ya shahidi;
   (d) yatakuwa na kurasa zenye namba mfululizo kama maelezo tofauti (au kama moja ya maelezo kadhaa yaliyomo kwenye jalada);
   (e) yatagawanywa katika aya zenye namba;
   (f) yataainisha namba zote kwa tarakimu, ikiwa ni pamoja na tarehe; na
   (g) yatatoa rejea ya nyaraka yoyote au zozote zilizotajwa katika pambizo au katika maandishi yenye wino mzito kwenye kiini cha maelezo hayo.

4.2. Maelezo ya shahidi yatafuata mlolongo wa matukio au masuala yanayoelezewa. Kila aya, kwa kadri itakavyowezekana, itajikita katika kipengele tofauti cha mada.

5. Tamko la Ukweli

5.1. Maelezo ya shahidi ni sawa na ushahidi wa mdomo ambao shahidi huyo angeutoa iwapo angeitwa kutoa ushahidi; lazima yajumuishe tamko la shahidi aliyekusudiwa kwamba anaamini taarifa zilizomo ndani yake ni za kweli.

5.2. Ili kuthibitisha maelezo ya shahidi tamko la ukweli litakuwa kama ifuatavyo: “Ninathibitisha kuwa taarifa zilizoelezwa katika maelezo haya ni za kweli”.

*6. Jurat*

Kila Kamishna wa viapo ambaye maelezo ya shahidi yamechukuliwa au kutolewa mbele yake ataandika jina lake na kueleza kwa ukweli katika *jurat* ya uthibitisho mahali ambapo na tarehe ambayo maelezo hayo yamechukuliwa au kutolewa na atagonga muhuri wake.

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 36)*

ADA

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Kufungua shauri | Tsh. 100,000/= |
| 2. | Kuwasilisha hati ya shauri iliyorekebishwa au kurekebisha hati ya shauri | Tsh. 50,000/= |
| 3. | Kuwasilisha majibu ya hati ya shauri | Tsh. 50,000/= |
| 4. | Kuwasilisha majibu ya hati ya shauri yaliyorekebishwa | Tsh. 50,000/= |
| 5. | Kuwasilisha maombi kwa ajili ya kuamua dhamana ya gharama za shauri | Tsh. 30,000/= |
| 6. | Kuwasilisha kiapo kinzani | Tsh. 10,000/= |
| 7. | Kuwasilisha orodha chini ya kanuni ya 13(1) | Tsh. 5,000/= |
| 8. | Kuwasilisha orodha ya malalamiko chini ya kanuni ya 14 (1) | Tsh. 5,000/= |
| 9. | Kuwasilisha nyaraka chini ya kanuni ya 19 | Ada sawa na inayopaswa kulipwa kwa suala kama hilo kwenye mashauri ya madai mahakamani |
| 10. | Kwa suala lingine lolote | Ada sawa na inayopaswa kulipwa kwa suala kama hilo kwenye mashauri ya madai mahakamani. |

Dar es Salaam,
16 Septemba, 2020

IBRAHIM HAMIS JUMA
*Jaji Mkuu*